

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAISI**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

SHULE YA SEKONDARI VUNTA  
S.L.P 83  
HEDARU SAME  
DESEMBA 2019  
Mob 0784792749/0764715952

Kumb Na VSS/SM/FS/10/2020/

MWANAFUNZI.....

S.L.P.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI VUNTA**  
**MWAKA 2021**

1.Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021, ambayo ni ya kutwa.Hii ni kutokana na wewe kufanya vizuri katika mtihani wako wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2020. Ni imani yangu kuwa utaitumia bahati hii vizuri kwa faida yako na Taifa lako.

Shule ya sekondari Vunta ipo umbali wa Km 70 Mashariki ya mji mkuu wa wilaya ya Same.

2.Shule kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza itafunguliwa tarehe 11/01/2021.

3.Iwapo unakubali uchaguzi huu ni lazima ufanye yafuatayo:

(i)Itakupasa uende kupima afya yako kwa mganga wa hospitali ya Serikali akishapima atakujazia fomu no 2 niliyoambatanisha na fomu hii

(ii) Itakupasa kujaza Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoingia kwenye migomo,fujo na makosa ya jinai.

(iii)Ni lazima mzazi /mlezi kujaza fomu ya kukiri kukubaliana na sheria,kanuni, na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

**4.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**  
**SARE**

**Wavulana**

i.Suruali mbili (2) za rangi brown "ugoro" (kitambaa kimeambatanishwa)

ii.Shati nyeupe mbili mikono mifupi aina ya tetroni

iii.Sweta moja la rangi ya brown "ugoro"

iv.Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba (gidamu) Sio Boots au Raba.

- v. Soksi jozi mbili (2) za rangi nyeupe au khaki
- vi. Sare za michezo kwa shule ni tracksuit ya blue bahari
- vii Raba jozi moja za michezo

### **Wasichana**

- i. Sketi mbili za rangi ya brown "ugoro" (kitambaa kimeambatanishwa)
- ii. Blauzi nyeupe mbili mikono mifupi aina ya tetroni
- iii. Sweta moja la rangi ya brown "ugoro"
- iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba visiwe vya visigino virefu
- v. Soksi jozi mbili (2) za rangi nyeupe au khaki
- vi. Sare za michezo kwa shule ni tracksuit ya blue bahari
- vii Raba jozi moja za michezo
- viii. Rangi ya hijabu kwa waisilamu ifanane na sare ya shule

### **5.VIFAA VYA TAALUMA**

- Daftari kubwa tisa (9) Quire two (2)
- Mkebe (Mathematical set 1)
- Mkoba wa daftari (usiwe wa Rambo)
- Kalamu na penseli
- Dictationary ya Kingereza kwa Kingereza (Oxford student's Dictionary 3rd Edition) Nimuhimu kila mwanafunzi awe nayo.

### **6.CHAKULA**

(i)Chakula cha wanafunzi kwa mhula ni

- kilo 18 za kande (mahindi yaliyokobolewa)
- maharage kilo 8 (Yasichanganywe na mahindi)
- Fedha ni Tsh 8,000

(ii)Mwanafunzi aje na sahani moja na kijiko kimoja kwa ajili ya kulia chakula

### **7.VIFAA VYA USAFI**

- a)Ufagio wa ndani mmoja ( kwa wote)
- b)Ufagio wa chelewa mmoja ( kwa wote)
- c) Panga moja kwa wavulana
- d)Jembe moja kwa wasichana
- e) Ndoo moja ya lita 10 kwa wote

NB: Vifaa ni muhimu sana ni lazima kila mwanafunzi aje navyo siku ya kuripoti, Aidha wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti pamoja na mzazi wake pamoja na vifaa hivyo vya usafi.

## **9. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

9:1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo.

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii  
Kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation)
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

### **9.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE**

- i) Wizi
- ii) Uasherati na Ushoga.
- iii) Ubakaji
- iv) Ulevi na Matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine mirungi na kubeli n.k
- v) Kupigana nakupiga.
- vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- vii) Kudharau bendera ya Taifa
- viii) Kuo au kuolewa
- ix) Kupata mimba au kutoa mimba ndani na nje ya shule.
- x) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- xi) Kukataa adhabu kwa makusudi
- xii) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

Nakutakia maandalizi mema  
Karibu Vunta Sekondari

.....  
**NZIAMWE N. NGEDU**

**MKUU WA SHULE**

**JAMUHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**  
**OFISI YA RAISI**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

SHULE YA SEKONDARI VUNTA  
S.L.P .83  
HEDARU

1. Kuandikishwa shule

( sehemu hii ijazwe na mwana funzi mwenyewe )

- (i) Jina kamili la mwanafunzi / majina matatu ( Tumia herufi kubwa)  
.....
- (ii) Tarehe ya kuzaliwa .....
- (iii) Mahali unapoishi:  
Kijiji.....  
Kata.....  
Tarafa.....
- (iv) Mahali anapoishi mzazi /mlezi  
Kijiji.....  
Kata.....  
Tarafa.....Mji.....
- (v) Anwani yako .....
- (vi) Jina kamili la mzazi/ mlezi .....
- (vii) Kazi za mzazi /mlezi .....

2. Kukubali nafasi ya masomo:

- (i) Mimi.....  
ambaye ni mwanafunzi niliye bahatika kuchaguliwa kuingia katika Shule hii ninaahidi yakuwa nitaitumia vyema nafasi hii kwa kusoma na kuzitii sheria za shule, nitadumisha nidhamu ndani na nje ya shule. Nakiri kwamba iwapo nitakiuka masharti hayo nichukuliwe hatua za kinidhamu kufuatana na taratibu ,kanuni na sheria zilizopo.

Sahihi ya Mwanafunzi.....

- (ii) Mimi .....ambaye ni  
mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu (sehemu ya (i) )  
ninakubali nafasi hii mwanangu kusoma naahidi yakuwa nitakuwa na ushirikano mzuri na uongozi wa shule ikiwa ni pamoja na kukamilisha karo na michango yote ya Shule kwa wakati unaohitajika.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

FROM HEADMASTER  
VUNTA SECONDARY SCHOOL  
P.O.BOX 83  
HEDARU

TO: THE MEDICAL OFFICER  
.....  
.....

RE:.....

(NAME OF STUDENT)

Please examine the above named as to his/her fitness for pursuing Secondary school Education. The Medical examinations may include the following areas.

- 1) Eye sight .....
- 2) Hearing.....
- 3) Leprosy.....
- 4) Limbs.....
- 5) Epilepsy.....
- 6) Asthima.....
- 7) T.B.....
- 8) Neuresis.....
- 9) Other illness (if any).....

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a medical officer)

I have examined the above student and consider that he/she is physically fit/unfit to pursue studies at secondary level

Date.....

Signature.....

Station.....

Designation.....

Official Stamp

**TAMKO LA MZAZI KUHUSU KUKUBALIANA NA KANUNI MASHARTI  
PAMOJA NA MICHANGO KWA MWANAFUNZI**

Mimi..... wa Kijiji  
cha.....nakiri kupokea kanuni na masharti ya mwanangu kujiunga na  
Shule ya Sekondari VUNTA.

Ninaahidi kuwa nitakuwa mstari wa mbele kulipa michango yote na mahitaji mengineyo  
ya Shule

Pia naahidi kwamba wakati wowote ndani ya miaka mine mwanangu hataacha shule kwa  
sababu yoyote ile labda iwe kwa amri ya daktari kuhusiana na afya yake au kuvunja  
sheria ya shule inayompasa afukuzwe Shule

.....  
Jina na Sahihi ya Mzazi/Mlezi

.....  
Jina na Sahihi ya Mtendaji Kijiji

.....  
Mhuri wa Ofisi

**N.B**

Fomu Na 1,2,3. Mwanafunzi aje nazo wakati wa kuripoti